

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI**

**19 MEI, 2026**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – TAREHE 19 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA UJENZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga

Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**372. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Zahanati Kijiji cha Zugumlole itakayohudumia Vitongoji vya Kaung'ando, Ibasu "A" na "B", Mkombozi, Ulinda na Ndevelwa.

**373. MHESHIMIWA DEVOTHA DANIEL MBURARUGABA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha Wabunge wa Viti Maalum wanashirikishwa katika utoaji wa Mikopo ya 10% kwenye Halmashauri.

**374. MHESHIMIWA DICKSON NATHAN LUTEVELE (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Stendi ya kisasa ya Mabasi Halmashauri ya Mji wa Mafinga.

**375. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuondoa mgongano wa Vikao vya Bunge na Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji ili Wabunge washiriki.

**OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):**

**376. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUWAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali imejipangaje katika kuzitafuta fursa za kuwawezesha Vijana.

## **WIZARA YA UCHUKUZI:**

### **377. MHESHIMIWA KASSIMU AMARI MBARAKA (TANGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Bandari ya Tanga - Kilimanjaro - Arusha - Singida hadi Musoma (Km 1108) utanza.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **378. MHESHIMIWA JOHN FRANCISCO NZILANYINGI (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya njia nne kutoka Mjini - Usagara na kutoka Mjini - Kisesa.

### **379. MHESHIMIWA EDIBILY KAZALA KINYOMA (KASULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itanza ujenzi wa Barabara ya Uvinza Kasulu na Makere- Nyarugusu – Kitanga kwa kiwango cha lami.

**380. MHESHIMIWA HARAN NYAKISA SANGA  
(KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kuna tofauti gani kati ya Daraja la Tanzanite na Daraja la Mwalimu Nyerere Kigamboni.

**WIZARA YA MAJI:**

**381. MHESHIMIWA TWAHA SAID MWAKIOJA  
(MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itafanya utafiti wa vyanzo vya uhakika vya maji Tarafa ya Maramba, Wilaya ya Mkinga ili kutatua changamoto ya maji kwa Wananchi.

**382. MHESHIMIWA ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE  
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Miradi ya Maji ya Tuwemacho, Masuguru-Mchoteka, Liwanga, Msingi na Azimio itakamilika.

**WIZARA YA FEDHA:**

**383. MHESHIMIWA LUCY EDWARD MWAKYEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa madeni ya Wakandarasi na Wazabuni.

**WIZARA YA AFYA:**

**384. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti watoa elimu ya afya na aina ya ulaji mitandaoni bila kuwa na Taaluma inayotambulika jambo linalowachanganya Wananchi.

**WIZARA YA KILIMO:**

**385. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza upatikanaji wa Mbegu bora na kwa bei nafuu nchini.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA  
19 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**

